Msururu wa Upotofu na Udanganyifu

# KUUFANYASHARIA UCHAFU

**Kutakasika Uislamu**
Kutokana na Madai ya wenye Fikra potevu ya kufaa Usuluhifu na Uchafu kwa kupotosha Neno la Allah Alietukuka: { Allah hapendi kujihirisha maneno mabaya ila Aliedhulumiwa, na Allah ni Mskizi na ni Mjuzi }



Toleo

3

SANAD

Sw

بسم الله الرحمن الرحيم

Kila jinsi ya sifa njema ni za Allah Mlezi wa Viumbe wote,
Rehma na Amani zimshukie mbora wa Manabii na Wajumbe,
Nabii wetu Bwana Muhammad na Jamaa zake na Swahaba zake wote.

## DINI YA UMARIDADI

## IMEJITOKEZA SAUTI GENI KATIKA ZAMA HIZI INAYODAI KUA USULUHIFU NA UCHAFU NA MATUSI YANA DALILI KUTOKANA NA QUR'ANI NA SUNNA!

Yajulikana wazi kua Uislamu umewalingania Waumini kusema Mazuri na kutenda ya kupendeza, na umewasisitiza wema na Tabia njema, na kuepuka machafu yaliodhahiri na yaliofichika.

Lakini yaweza mtu akauliza: Je Uislamu si umemruhusu Aliedhulumiwa kujihirisha Ubaya kwa Aliemdhulumu, kama vile katika neno la Allah Alietukuka: ﴿Allah hapendi kujihirisha maneno mabaya ila kwa Aliedhulumiwa, na Allah ni Mskizi na ni Mjuzi﴾ [1]

Mana imejitokeza Sauti Iliopotoka katika zama hizi inadai jambo la ajabu, kua Usuluhifu na Uchafu na Matusi, yana Dalili kutokana na Qur'ani na Sunna!

Lakini je inaingia akilini iwe katika Muongozo wa Allah Alietukuka na Mjumbe wake S.A.W. [Kuruhusu] Usuluhifu na Uchafu kwa Aliedhulumiwa katika kumrudi Aliemdhulumu?!



(1) An-Nisaa : 148


## Kukatika Mapokezi ➡ Kupotoka Ufahamu

Allah amemalizia Ujumbe wake kwa kumtumiliza Bwana wetu Muhammad Rehma na Amani ziwe juu yake na Jamaa zake, na akaihifadhi Dini baada yake kwa Wanazuoni wa Umma ambao waliipokea kwa Mapokezi yalioshikana, ndipo ukapokezanwa Ufahamu Sahihi wa Dini hini kwa Mapokezi haya, wala hapondoki kutokana na Ufahamu hunu ila alievamia ngome za Dini hini pasina Mapokezi haya.

### Wamefahamu nini wenye Fikra potofu kutoka kwa Aya kwa Aliedhulumiwa na Mwanadamu yoyote?

- Kua ana haki kumtusi na kumtukana na amtupie matamshi mabaya.
- Kua Matango na Matusi ndio asili katika kurudi [kulipiza] mabaya.

Lakini kudhania haki hini kumewapelekea kuendelea katika mfumo huu usiokua na Tabia



## Kukatika Mapokezi ➡ Kupotoka Ufahamu ➡ Fikra Gonjwa

Kisha wamemnasibishia Allah Alietukuka maneno Machafu na wakamnasibishia Mjumbe wake Mtukufu S.A.W. kuyafanyasharia, kwa kufata matamaniwa ya nafsi zisizotulia ila kujizulia vipengee vya kisharia vitakavowasaidia kutekeleza hasira na matamaniwa yake kwa ubaya wa tabia na maneno mabaya, kisha zidai kua hayo yafaa kisharia, bali yatakikana kufanya hivo!

### SHUBHA YA KWANZA

**Ushahidi:** Neno la Allah Alietukuka: ﴿Jeuri baada ya hayo ni Mwanaharamu﴾[2]

### Ufahamu Makosa:

Kutumia Sifa hizi Mbaya kwa yoyote kama asili wala sio kwa mtu Maalumu.

### Ufahamu Swahihi:

Sifa hizi zimefungamana na hali maalumu ili kubainisha uhakika uliokua umefichika kwa watu.
“Al-Etli Az-Zaniym’[3]maana yake ni Anaejidai Aliebandikwa na watu na si kati yao, nae [hapa] ni Walid bin Mughira, ama ni Anaejulikana kwa Shari.[4]

---

(2) Al-Qalam 13 .

(3) Mafatihul-Ghayb, Fakhrud-Diin Ar-Raaziy, Tafsiir Surat Al-Qalam (30/607) .

(4) Jamiul-Bayaan, At-Twabariy, Tafsiir Surat Al-Qalam (23/164) ; Tafsiir Ibnu Kathiir (8/212) ; Tafsiir Ibn Atwiya (5/347) ; Tafsiir Al-Qurtubiy (18/231) .

## SHUBHA YA PILI

**Ushahidi:** Neno la Allah Alietukuka: ﴿... Lakini yeye alipindukia Aridhini na akafuata hawaa zake, hivo mfano wake ni kama Mbwa ukimkimbiza anahema au ukimwachilia bado anahema, huo ndio mfano wa watu ambao wamekanusha Ishara yetu﴾[5]
Na neno lake Alietakasika: ﴿... Mfano wa wale waliobebeshwa Tawrati alafu wasi-ibebe [inavotakikana] ni kama mfano wa Punda anaebeba vitabu, mfano mbaya ni wa watu waliokanusha Ishara za Allah﴾[6]

### Ufahamu Makosa:

Kumuambatishia Allah alietukuka sifa ya upungufu ya aibu ambayo ni "Usuluhifu" na chanzo cha mkasa huu watokamana na kutofahamu misingi ya Lugha ya kiarabu katika kufananisha, na tafauti iliyoko baina yake na baina ya Sifa.

### Ufahamu Swahihi:

Lugha ya kiarabu ndio yenye uamuzi kwa mana ndio utamshi wa fikra zao, na katika Somo la Lugha ya kiarabu kuna kiswa cha yule Mshairi aliemsifu mmoja wa makhalifa kwa neno lake: "Wewe ni kama Mbwa katika kuchunga urafiki na ni kama Kondoo katika kuyatonga mikasa" na makusudiwa hapa ni zile sifa kutokana na mifano wala sio matusi na matukano.

Mungu amewapigia hawa mfano wa hali ya Punda anaebeba vitabu hana lengine ndani ya hivo vitabu ila ni kubeba bila kujua wala kufahamu. [7]
[Na yule mwengine] Ukimuedhea ye ashapota na ukimwachilia ye ashapotea, kama Mbwa ukimfukuza anahema na ukimwacha alivo anahema, mfano wake ﴿Na ukiwa-lingania kwenye Uongofu hawatawafuata sawa kwenu mukiwalingania ama mukiwanyamazia﴾ (Al-Aaraaf - 193)[8]

Lengo ni kuzifanya mbaya hali hizi na kuwaepusha watu nazo, na kuwalingania kwenye ukamilifu ulioko katika kufata maagizo ya kisharia na kumtwii Allah na Mjumbe wake.[9]

**Mkasa wa kumuambatishia Allah Alietukuka Sifa ya Usuluhifu chanzo chake ni kutokuwepo Ufahamu wa Misingi ya Lugha ya kiarabu katika kufananisha, na tafauti iliyoko beina ya kufananisha na baina ya kutoa kama Sifa.**

(5) Al-Aaraaf : 176 .
(6) Al-Jum'aa : 5 .
(7) Tafsiir At-Twabariy .
(8) Tafsiir Al-Baghawiy .
(9) Angalia : Tafsiir At-Tahriir wa At-Tanwiir, At-Twahir Ibn Ashuur (28/213) Tafsiir Zadul-Masiir, Abil-Faraj Al-Jawziy (4/281) ; Tafsiir Al-Qurtubiy (18/94) .

## JAMBO LA ASILI KATIKA MUONGOZO WA MTUMI

Sunna takatifu zimeweka wazi asili katika Tabia za Muislamu katika kuamiliana na Aliemkosea, miongoni mwazo ni :

Kutoka kwa Aisha R.A. : Kwamba Mayahudi walimjia Mtumi Rehma na Amani ziwe juu yake wakamwambia: "Maangamivu yawe juu yenu" Aisha akawajibu : "Na juu yenu, na Allah awalaani, na hasira za Allah ziwe juu yenu" Mtumi Akasema : (( Taratibu Aisha, Jilazimishe Upole, na jihadhari na vita na uchafu [wa maneno] )) Akasema Aisha: "Hukuskia walioyasema?" Mtumi akasema: (( Hukuskia nilivosema? Nimewarudishia juu yao, nitajibiwa mimi kwao, wala hawatojibiwa wao kwangu)).[10]

Kutoka kwa Abdallah bin Masuud Allah awe radhi nae Amesema : Amesema Mtumi S.A.W. : (( Muumini hawi Mtia wala Mtu wa kulaani wala Mchafu wala Msuluhifu )).[11]

Kutoka kwa Jaabir bin Sumura R.A. Amesema : Nilikua kwenye Kikao ndani yake yuko Mtumi Rehma na Amani ziwe juu yake, na Abi Samura amekaa mbele yangu, Akasema Mtumi Rehma na Amani ziwe juu yake : (( Hakika Uchafu na Kujifanya Mchafu si katika Uislamu, na hakika Mtu mwenye Uislamu mzuri zaidi ni mwenye Tabia nzuri zaidi )).[12]

### Kushikana Mapokezi ➡ Ufahamu Swahihi

Wanazuoni wa Umma wameifahamu ile Aya tukufu Ufahamu Swahihi wakaibainisha maana yake Ubainifu wakutosha, na haya ni Mkusanyiko wa Maneno ya Maswahaba na Waliowafuatia na Wafasiri juu ya Aya hiyo :

### Bingwa wa Umma Abdallah bin Abbaas Allah awe radhi nao (17 H) :

Amesema : Allah hapendi Mtu amuapize Mtu ila akiwa Amedhulumiwa, basi amemruhusu amuapize Aliemdhulumu, ndio neno lake : ﴿..ila Aliedhulumiwa..﴾ na akisubiri ni bora kwake.[13]

### Imaam Hasan Al-Baswariy (110 H) :

Amesema : Ni mtu anaemdhulumu mwenzake basi asimuapize, bali aseme : Ewe Mola nisaidie juu yake na unitolee haki yangu kwake,.
Na katika mapokezi kutoka kwake amesema : Ameruhusiwa amuapize Aliemdhulumu pasina kumfanyia uadui [kupta mipaka]. [14]

---

(10) Bukhariy, Mlango : Mtumi hakuwa Mchafu wala hakujifanya Mchafu, Hadithi ya 6030 .
(11) Tirmidhiy, Mlango : Yaliopokewa kuhusu Laana, Hadithi ya 1977 .
(12) Imepokewa na Ahmad, Musnadul-Baswariin, Hadithi ya Jaabir bin Abdallah : 20831 .
(13) Tafsiir Ibnu Kathiir, 2/442 .
(14) Marudio yaliotangulia .

### Imaam Mujaahid bin Jibr (104 H) :

Amesema : Ni Mtu anaemkirimu Mtu alafu nae asimkirimu, basi ameruhusiwa ataje aliyomtenda, yani [kwa kusema] : Hakunikirimu wala hakunipokea kama Mgeni.[15]

## Kushikana Mapokezi → Ufahamu Swahihi → Msururu wa kupokezana

Wanazuoni wa Umma wameafikiana juu ya Ufahamu huu Swahihi na kua Kusamehe ni bora, kando kabisa na Usuluhifu na maneno machafu ; na hayo ndio tunayoyapata katikaVitabu vya Tafsiri, miongoni mwazo kwa mfano :

### Wanazuoni walioifasiri ile Aya kwa Ufahamu Swahihi na Mapokezi yalionyoka :

| | |
|---|---|
| Tafsiri ya Ibnu Jurair At-Twabariy 310 H | Tfsiri ya Muqaatil 150 H |
| Tafsiri ya Az-Zajaaj 311 H | Tafsiri ya As-Swanaaniy 211 H |
| Tafsiri ya At-Thaalabiy 427 H | Tafsiri ya Ibnu Abi Haatim 327 H |
| Tafsiri ya Al-Baghawiy 510 H | Tafsiri ya As-Samaaniy 489 H |
| Tafsiri ya Bin Hayaan 745 H | Tafsiri ya Ibnu Atwiya 542 H |
| Tafsiri ya Ar-Raziy 606 H | Tafsiri ya Al-Jawziy 597 H |
| Tafsiri ya Annasafiy 710 H | Tafsiri ya Ibn Abdisalaam 660 H |
| Tafsiri ya Al-Qurtubiy 671 H | Tafsiri ya Al-Khaazin 741 H |
| Tfsiri ya Abu Suud 982 H | Tafsiri ya Al-Jalalaini 864 H |
| Tafsiri ya Al-Maraaghy 1371 H | Tafsiri ya M. S. Khaan 1307 H |



(15) Imepokewa na Ahmad, Musnadul-Baswariin, Hadithi ya Jaabir bin Abdallah : 20831 .

## Kukatika Mapokezi ➡ Kupotoka Ufahamu ➡ Fikra Gonjwa ➡ Mkasa

Upotofu unaanza kidogo ndio uendelee na upanuke ikiwa hautapatilizwa kwa kurudi kwenye Ufahamu wa Wanazuoni wa Umma wenye mapokezi yalioshikana, na kupanuka kwa kupotoka Ufahamu kunapelekea makosa na mikasa yanayoikosea Dini na wenye Dini.

### Ni zipi athari wazi za kuikosea Sharia kwa kueneza Ufahamu makosa?

- Kuenea kwa Matamshi machafu kwa hoja kua ndio asili katika Dini.
- Kutikisika imani juu ya mfumo wa kitabia wa kiislamu uliotukuka, ndani ya Nyoyo za watu.
- Kupewa sifa Uislamu kutoka kwa Maadui zake na hata baadhi ya Waislamu, kua ni Dini inayozifanyasharia Tabia mbaya na Matamshi machafu.
- Kudhania makosa wengi wa vijana wa Kiislamu kua kumtusi Dhalimu na kumtukana na kumtupia maneno Machafu haina neno kiupande wa Sharia na kua ndio inavotakikana.

Amesema Hasan Al-Baswariy

**Asimuapize, bali aseme**

(Ewe Mola nisaidie juu yake
na unitolee haki yangu kwake)



## KWA UFUPI

- Uislamu waamrisha Maneno mazuri na unayasisitiza katika hali zote za Kibinadamu pamoja na Wanadamu wenzake.

- Asili ya kimsingi katika Dini ya unyenyekevu [Uislamu] kukataza Ulimi mchafu na Maneno mabaya.

- Ni ya hatari wanayoyadai baadhi ya wanavikundi vipotofu, kua kumtupia Dhalimu Matamshi machafu ni jambo limethibitishwa katika Sharia ; na makosa makubwa zaidi ni kukimbilia kuufanyasharia Ulimi mchafu waliokotana nao wengi kati yao.

- Hapama budi kurudi kwa viongozi wa kidini wanaotambulika katika kufahamu maandishi ya kisharia ili Muislamu asiangukie kwenye tope za upotevu wadanganyifu wenye malengo na hawaa na muono mfupi.

- Ni muhimu sana kuwalinda Vizazi vya kiislamu kutokamana na mchezo wa wanaokimbilia kuichafua Dini na kuitweza kwa kujaribu Kuufanyasharia Uchafu na Usuluhifu katika kupambana na Madhalimu, ili isitingishike jengo la kiislamu baina ya turathi zinazosisitiza Tabia nzuri na wanaojidai udini wanaofanya Tabia mbaya.

- Hakuna dalili kwenye Aya hini tukufu : ﴿ Allah hapendi kujihirisha maneno mabaya ila Aliedhulumiwa, na Allah ni Mskizi na ni Mjuzi ﴾ Kufaa Uchafu wowote ama Usuluhifu katika kumrudi Dhalimu, ama kumtweza kwa kumtupia maneno mabaya ambayo yamekatazwa na Dini yetu nyenyekevu kimsingi kama ilivotangulia.

(( Je si haitawatumbukiza watu kwa nyuso zao ndani ya Moto ila matumo ya Ndimi zao ))

Hadithi Tukufu [16]



(16) Ameipokea Ahmad na Tirmidhiy na akasema ni Hadithi Nzuri Swahihi .

# MSURURU WA UPOTOFU NA UDANGANYIFU

Amesema Mjumbe wa Allah Rehma na Amani ziwe juu yake na jamaa zake : (( wataichukua hini Elimu [Dini] Waadilifu katika kila watakaokuja, watakaoitetea kutokana na Upotofu wa Wenye kuzidisha na Udanganyifu wa Wenye kuharibu na Ufafanuzi wa Wajinga )) [1]

Wamefahamu baadhi ya wenye fikra za makosa, maneno ya Allah Mtakatifu na Mtumi wake S.A.W. kwa namna hailingani na mfumo wa kielimu uliopokewa kutoka kwa waliotangulia wema, wala kuchukuana na makusudio na misingi mikubwa ya Ujumbe wa Mungu.

Wakazichukua kusudi baadhi ya Aya za Qur'ani Tukufu ambazo ziliteremka kwa wasiokua Waislamu wakaziteremsha kwa Waislamu, na wakachukua Aya ambazo zimekuja si kwa jumla wakazifanya ni Maagizo ya kwa jumla.
Na wakapotosha maana ya Maneno ya Allah na Hadithi za Mtumi wake Mtukufu kwa namna imepelekea kukita kwa ufahamu wa kimakosa sana ndani ya akili za Waislamu wasiowasomi, uliowapelekea kwenye nyendo na vitendo havina ufungamano na Dini ya Unyenyekevu ya Kiislamu.

Tutajua kupitia Msururu huu, Upotoshaji wa maana ya Maneno ya Allah na Mtumi wake, waliouangukia wenye fikra hizi za makosa, na kutilia nguvu kwao Fahamu za makosa, kiasi kilichowafanya wawe kando na Makusudio ya Allah na Mtumi wake na Ufahamu wa Wema waliotangulia .

(1) Hadithi mash'huri ameiswahihisha Ibn Abdil Bar, na amepokewa Ahmad bin Hanbal kua Amesema: hio ni Hadithi Swahihi .


DAR AL FAQIH
PUBLICATION & DISTRIBUTION

SANAD

www.sanad.network
twitter: @sanadnetwork
facebook.com/sanadnetwork
youtube.com/sanadnetwork
instagram.com/sanadnetwork